# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA



# MWONGOZO WA ULINZI NA USALAMA KATIKA VYUO VYA MAENDELEO YA WANANCHI, VYUO VYA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI NA VYUO VYA UALIMU

# DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepiga hatua katika kuimarisha mifumo ya utoaji wa elimu bora na jumuishi kwa wote. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza fursa za elimu kwa usawa na kuinua kiwango cha ubora wa Elimu inayotolewa katika ngazi zote. Lengo ni kukuza maarifa na ujuzi utakaomwezesha mhitimu kujiajiri au kuajiriwa.

Serikali kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, imeweka miundo, mipango, mikakati na taratibu zinazohakikisha upatikanaji wa elimu na mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu nchini. Matokeo ya utekelezaji wa Sera hii ni kuwa na mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 imeandaa Mpango wa Maendeleo katika Sekta ya Elimu 2021/22 - 2025/26. Mpango huo unabainisha mipango mipya ya kukidhi mahitaji ya sasa ya ujuzi na vipaumbele vya Serikali pamoja na kutatua changamoto zinazozuia upatikanaji wa elimu bora, yenye usawa, na jumuishi katika Vyuo vya Maendeleo ya wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu nchini.

Kutokana na umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi na Elimu ya Ualimu Nchini, ni muhimu kuzingatia ushiriki wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika kupata maarifa, ujuzi na mtazamo chanya. Pamoja na hatua zilizochukuliwa katika kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupata fursa ya Elimu, bado wengi wanakabiliwa na changamoto za kielimu katika kufikia ndoto zao. Baadhi ya changamoto hizo ni unyanyasaji na ukatili kwenye jamii. Hivyo, jitihada za makusudi zinahitajika ili kukabiliana na changamoto hizo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na Serikali ya Kanada kupitia Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Kanada imeandaa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa Wanachuo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu.

Mwongozo huu umeainisha mikakati ya utekelezaji na kutoa maelekezo kwa wadau ili kuweka kipaumbele katika ulinzi, usalama na ustawi wa wanachuo. Hivyo, Wizara

inatarajia kuwa vyuo husika, wadau na washirika wa maendeleo watatumia mwongozo huu kuimarisha ulinzi na usalama ili kupunguza vitendo vya ukatili na unyanyasaji.

Prof. Carolyne I. Nombo

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

## SHUKURANI

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inawashukuru wataalamu kutoka Wizara mbalimbali kwa kushiriki katika maandalizi ya Mwongozo huu.

Shukurani zinatolewa kwa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu, na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa maoni na ushauri.

Shukurani za kipekee zinatolewa kwa Serikali ya Kanada kwa kufadhili uandaaji wa Mwongozo huu kupitia Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Kanada inayotekeleza Mradi wa Uwezeshaji kupitia Ujuzi (Empowerment through Skills Program - ESP).




Dkt. Lyabwene M. Mutahabwa

**KAMISHNA WA ELIMU**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# YALIYOMO


**DIBAJI** ........ ii
**SHUKURANI** ........ iv
**Vifupisho** ........ vii
**SURA YA KWANZA** ........ 1
1.0 UTANGULIZI ........ 1
1.1 Sheria, Kanuni na Taratibu ........ 2
1.1.1 Kanuni ya Adhabu ........ 2
1.1.2 Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, (Kifungu 29) ........ 2
1.1.3 Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18 – 2021/22 ........ 2
1.2 Chimbuko la Mwongozo ........ 2
1.3 Malengo ya Mwongozo ........ 4
1.3.1 Lengo kuu ........ 4
1.3. 2 Malengo Mahususi ........ 4
1.4 Wigo wa Mwongozo ........ 4
1.5 Walengwa wa Mwongozo ........ 4
1.6 Wanufaika ........ 5
1.6.1 Wanufaika wa Moja kwa Moja ........ 5
1.6.2 Wanufaika Wasio wa Moja kwa Moja ........ 5
**SURA YA PILI** ........ 6
2.0 DHANA ZINAZOHUSIANA NA JINSIA NA UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU ........ 6
2.1 Jinsia ........ 6
2.2 Unyanyasaji wa kingono ........ 6
2.3 Ulinzi ........ 6
2.4 Unyanyasaji ........ 6
2.5 Ubaguzi ........ 6
2.6 Ukatili wa Kijinsia ........ 7
2.7 Unyanyasaji wa Kimwili ........ 7
2.8 Unyanyasaji wa kisaikolojia ........ 7
2.9 Unyanyasaji wa kingono ........ 7
2.10 Unyonyaji wa kingono ........ 8
2.11 Ukatili wa kimwili ........ 8
2.12 Ukatili wa kisaikolojia ........ 8
2.13 Ukatili wa maneno ........ 8
2.14 Ukatili wa kingono ........ 8
2.15 Kutelekezwa ........ 8

2.16 Unyonyaji ..... 9
2.17 Uonevu ..... 9
2.18 Madhara ..... 9
2.19 Ufuatiliaji ..... 9
2.20 Tathimini ..... 9
**SURA YA TATU ..... 10**
3.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI NA UENDELEVU ..... 10
3.1 Lengo 1 ..... 10
3.2 Lengo la 2 ..... 11
3.3 Lengo la 3 ..... 13
3.4 Lengo 4 ..... 16
**SURA YA NNE ..... 17**
4.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO ..... 17
4.1 Mifumo ya Usimamizi na taratibu za Ulinzi, usalama. ..... 17
4.2 Majukumu na Wajibu wa Wadau. ..... 18
4.2.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ..... 18
4.2.2 Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) ..... 18
4.2.3 Bodi za Vyuo ..... 19
4.2.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa ..... 19
4.2.5 Menejimenti za vyuo ..... 19
4.2.6 Washirika wa Maendeleo ..... 20
4.2.7 Mashirika yasiyo ya Kiserikali ..... 20
4.2.8 Sekta Binafsi ..... 20
4.2.9 Wazazi/Walezi na Jamii ..... 20
4.2.10 Watumishi wa Vyuo ..... 21
4.2.11 Uongozi wa Wanachuo ..... 21
4.2.12 Mwanachuo ..... 21
**SURA YA TANO ..... 22**
5.0 Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji ..... 22
5.1 Ufuatiliaji na Utoaji wa Taarifa ..... 22
5.2 Tathmini ..... 22
5.3 Ujifunzaji ..... 23
**KIAMBATISHO 1: MPANGO WA UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI. ..... 24**

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AZAKI** | Asasi za Kiraia |
| **CEDAW** | Convention for Elimination of All Forms of Discrimination Against Women (Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake) |
| **CICan** | Colleges and Institutes Canada (Jumuiya ya Vyuo na Taasisi za Ufundi Kanada) |
| **ESP** | Empowerment through Skills Program (Programu ya Uwezeshaji kupitia Ujuzi) |
| **NPAVAWC** | National Plan of Action to End Violence Against Women and Children (Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto) |
| **OR-TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. |
| **SOSPA** | Sexual Offences Special Provisions Act (Sheria ya Makosa ya Kingono) |
| **UN** | United Nations (Umoja wa Mataifa |
| **UNICEF** | United Nations International Children’s Emergency Fund (Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto) |
| **UKIMWI** | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| **VVU** | Virusi vya Ukimwi |

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, inatekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu hususani lengo namba Nne (4) linalohusu kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora ambayo ni jumuishi, yenye usawa na kukuza fursa endelevu za kujifunza kwa wote.

Sanjari na lengo namba Nne (4) la Malengo ya Maendeleo Endelevu, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 inasisitiza upatikanaji wa elimu na mafunzo kwa kila Mtanzania bila kujali jinsi, rangi, kabila, dini, ulemavu, jamii au kipato. Vilevile, Sera hii inasisitiza Serikali kuongeza fursa mbalimbali za elimu na mafunzo kwa makundi yote ya kijamii katika ngazi zote wakiwemo watoto, wasichana, wanawake na watu wenye ulemavu. Sambamba na hilo, Sera hii inaitaka Serikali kuondoa vikwazo vinavyozuia fursa za wanachuo kuendelea na masomo na kukamilisha mzunguko wa elimu kwenye ngazi husika.

Aidha, Ibara ya 10 (f) ya Mkataba wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi Dhidi ya Wanawake (1979) (Convention on the Elimination of all forms of Discrimination Against Women-CEDAW), inazitaka nchi ambazo ni wanachama, ikiwemo Tanzania, kuchukua hatua stahiki zitakazopunguza kiwango cha kuacha shule na kuwa na mpango mahususi wa kuwarudisha wasichana waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, lengo namba Tano la Malengo Endelevu ya Kiulimwengu linasisitiza zaidi nchi kuchukua hatua zote muhimu za kuimarisha usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na uwezeshaji wa wanawake.

Vilevile, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inahakikisha uhuru, haki, udugu, amani, utu wa binadamu, na kuondoa aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, rushwa, ukandamizaji, au upendeleo. Ibara ya 11-24 ya Katiba inaorodhesha haki kadhaa ambazo wananchi wanastahili. Haki hizo ni pamoja na usawa, haki ya kuishi, haki ya uhuru wa dhamiri, na haki ya kufanya kazi. Pia, kifungu cha 11 (2) cha Katiba kinaeleza kuwa kila mtu ana haki ya kupata elimu, na kila raia ana uhuru wa kupata elimu katika nyanja ya uchaguzi wake hadi kufikia kiwango cha juu kulingana na uwezo wake.

### 1.1 Sheria, Kanuni na Taratibu

Serikali ina Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Ulinzi, Usalama na Ustawi wa jamii wakiwemo watoto, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Miongoni mwa mifumo hiyo ni:

#### 1.1.1 Kanuni ya Adhabu

Mnamo Mwaka 1998, Bunge lilipitisha vifungu maalum vya makosa ya kujamiiana (Sheria ya Mwaka 1998) (Sexual Offenses Special Provisions Act-SOSPA) ambavyo vilirekebisha vifungu kadhaa vya kanuni za adhabu, ili kuongeza adhabu kwa makosa ya ubakaji na aina zote za unyanyasaji wa kijinsia. Sheria hiyo ililenga kufanya aina zote za unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto kuwa makosa ya jinai.

#### 1.1.2 Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971, (Kifungu 29)

Sheria ya Ndoa imeweka vifungu vinavyotetea haki za wanawake na wasichana ambavyo ni pamoja na amri dhidi ya unyanyasaji (Kifungu cha 139), kukataza kulazimisha mwanamke kurithiwa (Kifungu cha 68) na mgawanyo wa mali zilizopatikana wakati wa ndoa (kifungu cha 114).

#### 1.1.3 Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto 2017/18 – 2021/22

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum iliandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Miaka Mitano wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22). Mpango huu uliandaliwa kwa kujumuisha mipango nane (8) tofauti ya utekelezaji inayoshughulikia ukatili dhidi ya wanawake na watoto ili kuunda Mpango Kazi mmoja wa Kitaifa wa Utekelezaji katika kutetea yafuatayo:

i. Marekebisho ya sheria kadhaa kama vile Kanuni ya Adhabu ya Makosa ya Jinai, Sheria ya Ushahidi, na Sheria ya Ndoa.
ii. Kuundwa kwa dawati la jinsia katika kila Wizara
iii. Kuundwa kwa dawati la jinsia kupitia mtandao wa polisi wanawake ili kupokea na kushughulikia kesi za ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

### 1.2 Chimbuko la Mwongozo

Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Demografia Tanzania wa mwaka 2010, asilimia 39 ya wanawake wenye umri wa miaka 15-49 wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili

tangu wakiwa na umri wa miaka 15 na karibu theluthi moja ya wanawake (33%) wenye umri wa miaka 15-49 walifanyiwa ukatili wa kimwili katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti huo. Hii inaonesha kwamba karibia wanawake wanne kati ya kumi wamepitia unyanyasaji wa kimwili, na mmoja kati ya wanawake watano wanaripoti kufanyiwa unyanyasaji wa kijinsia katika maisha yao (kutoka umri wa miaka 15).

Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza barani Afrika kufanya utafiti wa Kitaifa kuhusu ukatili dhidi ya watoto ili kupima aina zote za ukatili ikiwemo ukatili wa kingono, kimwili na kihisia miongoni mwa wasichana na wavulana na kutoa makadirio ya Kitaifa ya kuenea kwa ukatili.

Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa Ukatili dhidi ya Watoto ya mwaka 2011 uliofanywa na Serikali ya Tanzania na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) uligundua kuwa karibu msichana mmoja kati ya watatu na mvulana mmoja kati ya saba walifanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kufikisha miaka 18. Ripoti hii inaonesha kuwa watoto wengi hawatoi taarifa za ukatili, wachache hutafuta huduma, na wachache zaidi hupokea huduma za matibabu na uangalizi ikiwa wataripoti unyanyasaji. Viwango vya ukatili wa kimwili na kihisia kwa wasichana ni asilimia 73.5 na kwa wavulana asilimia 71.7 wamepitia aina fulani ya ukatili wa kimwili.

Kutokana na matokeo hayo, serikali iliandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa miaka 5 wa kuzuia na kukabiliana na Ukatili dhidi ya Watoto (2011–2015) na baadaye kuandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa kukomesha ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto wa 2017/18 – 2021-2022.

Licha ya jitihada hizi, matukio ya uonevu, unyanyapaa, ubaguzi, unyanyasaji wa kijinsia, na aina nyingine za ukatili dhidi ya wanachuo hasa wanawake, vijana, na wenye ulemavu bado ni changamoto katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu. Changamoto hizi zimekuwa na athari katika ustawi wa kimwili na kisaikolojia kwa wanachuo hasa wanawake, vijana na wenye ulemavu. Hii ni kwa sababu changamoto hizi huathiri mahudhurio, utendaji wa kitaaluma, na hivyo husababisha kuongezeka kwa wanachuo kukatiza mafunzo vyuoni.

Hivyo, utekelezaji mzuri wa mwongozo huu utaboresha maarifa, ujuzi na mitazamo ya wanachuo, watumishi, na wadau wengine wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na

Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi juu ya ulinzi na usalama dhidi ya changamoto zinazowakabili. Changamoto hizo ni pamoja na ubaguzi, ulawiti, unyanyasaji wa kihisia, kimwili na kingono, ndoa za utotoni, uonevu, kukataliwa, na vitendo vingine vya kitamaduni vyenye madhara. Pia Mwongozo huu utaweka mazingira wezeshi yanayozingatia jinsia, ili kuwasaidia wanachuo wote hasa wanawake, vijana na wenye ulemavu.

### 1.3 Malengo ya Mwongozo

#### 1.3.1 Lengo kuu

Mwongozo huu unalenga kutoa maelekezo kwa wadau ili kukuza na kuweka kipaumbele katika ulinzi, usalama na ustawi wa wanachuo kwenye Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu.

#### 1.3. 2 Malengo Mahususi

1. Kuimarisha ulinzi na usalama wa wanachuo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu dhidi ya aina yoyote ya ukatili.
2. Kuanzisha/ kuboresha huduma saidizi ili kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama.
3. Kuanzisha mfumo sahihi wa kukabiliana na ukatili kupitia utaratibu salama wa kutoa taarifa**.**
4. Kujenga uelewa juu ya masuala ya usalama kwa wadau wote wenye mahusiano ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja na wanachuo.

### 1.4 Wigo wa Mwongozo

Mwongozo huu utahusisha wanachuo, wakufunzi, watumishi, wanaojitolea katika Vyuo vya Maendeleo ya Wanachi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Vyuo vya Ualimu pamoja na wadau wengine. Mwongozo huu utatekelezwa katika mipango na ratiba za chuo za kila siku.

### 1.5 Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa Mwongozo huu ni:

(i) Wanachuo

(ii) Uongozi wa Vyuo
(iii) Bodi za Vyuo
(iv) Watumishi wa Vyuo
(v) Wazazi/walezi/waangalizi wa wanachuo
(vi) Wadau wengine

### 1.6 Wanufaika

Wanufaika wa Mwongozo wamegawanyika katika makundi mawili; wanufaika wa moja kwa moja na wasio wa moja kwa moja. Wanufaika wa kila kundi wanatambuliwa kama ifuatavyo:

#### 1.6.1 Wanufaika wa Moja kwa Moja

i. Wanachuo (wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu).

#### 1.6.2 Wanufaika Wasio wa Moja kwa Moja

i. Wazazi /walezi wa wanachuo
ii. Uongozi wa chuo
iii. Bodi ya chuo
iv. Wasimamizi wa vyuo
v. Watumishi wa vyuo.
vi. Jamii inayozunguka vyuo
vii. Wadau wa maendeleo katika sekta ya elimu

**SURA YA PILI**

## 2.0 DHANA ZINAZOHUSIANA NA JINSIA NA UFAFANUZI WA MANENO MUHIMU

Utekelezaji madhubuti wa Mwongozo huu unahitaji uelewa wa kina wa dhana za kijinsia, maneno yanayotumika, na mienendo inayoweza kuathiri nyanja za maisha ya watu katika jamii. Uelewa wa masuala haya unaweza kuwasaidia watumiaji wa Mwongozo huu ambao ni watumishi, wanachuo na wadau wengine kutumia mamlaka yao ipasavyo na kubadilisha mienendo ndani na nje ya madarasa ili kila mwanachuo aone amewezeshwa, amethaminiwa, na kuwekwa salama katika mafunzo na ukuaji wake.

### 2.1 Jinsia

Dhana ya Jinsia inahusu majukumu, tabia, shughuli, na sifa ambazo jamii fulani kwa wakati fulani inaona zinafaa kwa wanaume na wanawake au wavulana kwa wasichana.

### 2.2 Unyanyasaji wa kingono

Unyanyasaji wa kingono ni aina ya unyanyasaji unaohusisha matumizi ya lugha za wazi za kingono, ikiwa ni pamoja na viashiria vya kutaka ngono pasipo ridhaa, ubakaji, maombi ya upendeleo kutokana na jinsi, na unyanyasaji mwingine wa maneno au ishara za kimwili.

### 2.3 Ulinzi

Ulinzi unaashiria hatua za kulinda afya, ustawi, na haki za binadamu, ambazo zinaruhusu watu hasa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kuishi bila unyanyasaji.

### 2.4 Unyanyasaji

Tabia mbalimbali zinazosababisha athari au zinazoweza kutokea kwa afya ya mtoto au kijana, ustawi, uhai, maendeleo, au heshima. Inajumuisha kitendo chochote au kushindwa kuzuia vitendo vya hatari kwa makusudi na kusababisha kifo au madhara mengine. Unyanyasaji unaweza kuwa wa kimwili, kihisia, au kingono.

### 2.5 Ubaguzi

Ubaguzi ni hali au uamuzi wa kumtendea mtu au kikundi vibaya kwa sababu ya rangi, umri, jinsi, dini, utaifa, au ulemavu.

Ubaguzi hutokea pale mtu anaposhindwa kufurahia haki zake za kibinadamu au haki nyingine za kisheria kwa misingi sawa na wengine kwa sababu ya tofauti isiyo ya haki kisera, kisheria, au kiutaratibu.

**2.6 Ukatili wa Kijinsia**

Ukatili wa kijinsia ni neno la jumla linalotumika kumaanisha tendo lolote lenye madhara linalofanywa kinyume na matakwa ya mtu. Tendo hilo linatokana na tofauti za kijamii (jinsia) kati ya wanawake na wanaume.

Asili na kiwango cha aina za ukatili wa kijinsia hutofautiana kulingana na tamaduni, nchi, na kanda. Mifano ni pamoja na unyanyasaji wa kingono, ukahaba wa kulazimishwa, ukatili majumbani, usafirishaji haramu wa binadamu, ndoa za kulazimishwa, ndoa za utotoni, vitendo vya kitamaduni vyenye madhara kama vile ukeketaji wa wanawake na urithi wa wajane.

**2.7 Unyanyasaji wa Kimwili**

Matumizi ya makusudi ya nguvu ambayo husababisha majeraha halisi au uwezekano wa kuumia kimwili au mateso (ambayo hayawezi kuonekana). Unyanyasaji wa kimwili unaweza kujumuisha, kutikiswa, kufinywa, kukabwa, kung`awta, kuchomwa moto, kupigwa ngumi, kurushiwa vitu na kupewa sumu. Vitendo hivyo ni unyanyasaji bila kujali kama vinalenga kusababisha majeraha.

**2.8 Unyanyasaji wa kisaikolojia**

Unyanyasaji wa kisaikolojia ni aina ya unyanyasaji ambao mtu anamfanyia au kumuweka mtu mwingine kwenye tabia ambayo inaweza kusababisha maumivu ya kisaikolojia, ikiwa ni pamoja na wasiwasi, sonona, sonona sugu, au msongo baada ya janga

**2.9 Unyanyasaji wa kingono**

Unyanyasaji wa kingono ni kitendo au jaribio la kutumia udhaifu, matumizi mabaya ya nafasi, mamlaka, au uaminifu kwa madhumuni ya kingono. Hii ni pamoja na kulazimisha, au kumshawishi mtu kushiriki katika aina yoyote ya vitendo vya kingono, kama vile kumuingilia, ubakaji, ngono ya mdomo, kumshika bila ridhaa, kutumia lugha ya wazi ya kingono au kuonyesha picha za ngono za mtu, ndoa za mapema au za kulazimishwa, ukahaba wa kulazimishwa, na utumwa wa kingono.

### 2.10 Unyonyaji wa kingono

Unyonyaji wa kingono unahusu kitendo halisi cha unyanyasaji au jaribio la unyonyaji wa kingono kwa kutumia udhaifu wa mtu.

### 2.11 Ukatili wa kimwili

Ukatili wa kimwili ni kitendo cha kujaribu au kusababisha maumivu na / au jeraha la kimwili. Ni pamoja na kupiga, kuchoma, kuuma, kuumiza, matumizi ya vitu au silaha, au kuvuta nywele. Kwa kiasi kikubwa, ukatili wa kimwili unaweza kusababisha mauaji. Ukatili wa kimwili pia ni pamoja na usafirishaji haramu wa binadamu na utumwa na mara nyingi vijana wa kike na wa kiume wanaohusika huishia kuwa wahanga wa unyanyasaji.

### 2.12 Ukatili wa kisaikolojia

Ukatili wa kisaikolojia unaweza kujumuisha, tabia za kutishia ambazo hazihusishi unyanyasaji wa kimwili au hata unyanyasaji wa maneno. Inaweza kujumuisha vitendo vinavyorejelea vitendo vya zamani vya ukatili, au kupuuza kwa makusudi na kutelekeza wengine. Ukatili wa kisaikolojia pia unaweza kufanywa kwa njia ya kutengwa au kufungwa, kuzuia habari, na upotoshaji.

### 2.13 Ukatili wa maneno

Ukatili wa maneno unaweza kujumuisha kudhalilishwa kwa faragha au mbele ya wengine, kejeli, matumizi ya maneno yasiyofaa ambayo yana mweka mtu katika hali isiyopendeza, kutishia na aina nyingine za unyanyasaji dhidi ya mwathirika, kitu au mtu wa karibu. Mara nyingine unyanyasaji wa maneno unahusiana na historia ya mwathirika, kumtukana, au kumtishia kwa misingi ya dini, utamaduni, lugha, (inayotambulika) au mila na desturi.

### 2.14 Ukatili wa kingono

Ukatili wa kingono ni kitendo au jaribio la kumuingilia mtu kimwili bila ridhaa yake. Vitendo hivi humuumiza kila mwathirika na hutumika vivyo hivyo katika nyanja za umma na faragha. Mifano ni pamoja na ubakaji baina ya wanandoa, jaribio la ubakaji, ngono isiyo salama, unyanyasaji wa kijinsia, kwa upande wa wanawake, na unyanyasaji unaohusiana na uzazi.

### 2.15 Kutelekezwa

Kutelekezwa kuna maanisha kushindwa kuendelea kukidhi mahitaji ya msingi ya kimwili /kisaikolojia ambayo husababisha madhara halisi yanayoweza kutokea kwa

afya ya mtoto, kijana, mwanamke na mtu mwenye ulemavu katika ustawi, kuishi, maendeleo, au heshima yake. Ni pamoja na kutenda kwa njia ambazo zinashindwa kumlinda mtoto au kijana dhidi ya hatari ambazo zinaweza kumweka mtoto au kijana katika hatari kubwa ya ukatili au kunyanyaswa.

### 2.16 Unyonyaji

Unyonyaji unahusu hali yoyote ambayo mnyanyasaji hutumia fursa ya mamlaka / hali duni ya kiuchumi ya mtu mwingine kujinufaisha, kupata kazi, kujifurahisha kingono au kifedha.

### 2.17 Uonevu

Uonevu ni tabia ya uchokozi ambapo mtu kwa makusudi kabisa na mara kwa mara humsababishia mtu mwingine ukosefu wa furaha na amani. Jambo hili huathiri sana afya ya kimwili na kiakili kwa mhanga. Watu wanaofanyiwa uonevu mara nyingi hupata shida kujitetea katika mazingira ya aina fulani.

### 2.18 Madhara

Madhara ni tabia zote mbaya / au tabia ambayo husababisha madhara ya kimwili au kisaikolojia, kwa mfano, unyanyasaji na vitisho, kusababisha hofu, au dhiki. Madhara yanaweza kusababishwa na unyanyasaji, kutelekezwa au unyonyaji kwa kukusudia au bila kukusudia.

### 2.19 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji ni shughuli inayojirudia mara kwa mara kuanzia katika hatua za upangaji wa mradi au programu. Ufuatiliaji unaruhusu matokeo, michakato, na uzoefu kuandikwa na kutumika kama msingi wa kufanya maamuzi na kujifunza. Ufuatiliaji unaangalia maendeleo dhidi ya mipango. Taarifa zinazopatikana kupitia ufuatiliaji hutumiwa kufanya tathmini.

### 2.20 Tathimini

Ni utaratibu wa kupima na kuchunguza hali halisi kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia kufanya maamuzi ya kimkakati yanayohusu uboreshaji masuala mbalimbali.

## SURA YA TATU

## 3.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI NA UENDELEVU

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu vinaelekezwa kutekeleza Mwongozo huu kama sehemu ya utekelezaji wa shughuli na mipango ya kawaida ya kila siku. Sura hii inatoa mwongozo kwa wadau juu ya mipango na mikakati ambayo inapaswa kutekelezwa ili kuhakikisha Ulinzi na Usalama wa wanachuo. Utekelezaji madhubuti wa mikakati hiyo itawawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kunufaika na mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia.

Ili kufikia lengo hili, malengo mahususi matano yameandaliwa ili kuongoza utekelezaji wa mwongozo wa Ulinzi na usalama. Kila lengo lina mikakati kadhaa ya utekelezaji kama ifuatavyo:

### 3.1 Lengo 1: Kuimarisha ulinzi na usalama wa wanachuo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu dhidi ya aina yeyote ya ukatili.

**Maelezo ya Lengo**

Mazingira yasiyofaa yanaweza kuathiri ufundishaji na ujifunzaji pamoja na maendeleo ya wanachuo vyuoni. Hivyo, kuna haja ya kuweka mazingira rafiki ambapo wanachuo, watajisikia salama na kulindwa wanapoendelea na masomo au shughuli zao. Ni muhimu kuweka mikakati inayowahakikishia ulinzi na usalama wao dhidi ya aina zote za ukatili vyuoni na mazingira yanayowazunguka**.**

**Mkakati: Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa ulinzi na usalama:**

**Tamko la Mkakati**

Wanachuo, hasa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, wako katika hatari zaidi ya kukumbana na aina mbalimbali za ukatili, unyanyasaji, na madhara nyumbani, njiani kwenda vyuoni na vyuoni. Kwa hiyo, mfumo wa huduma ya ulinzi na usalama lazima uwekwe ili kuwalinda dhidi ya vitendo hivyo na kutoa utaratibu

sahihi na ulio salama wa kutoa taarifa. Ili kuhakikisha ulinzi na usalama wa wanachuo, vyuo vinapaswa kuzingatia yafuatayo: -

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. Kuzingatia na kutekeleza Miongozo mbalimbali ya Serikali inayohusiana na haki za wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.
ii. Kuajiri walinzi wenye umahiri na wa kuaminika ili kudumisha ulinzi na usalama.
iii. Kuzingatia na kukuza upatikanaji wa miundombinu rafiki kwa watumiaji wote wakiwemo watu wenye ulemavu katika mazingira ya chuo
iv. Kuimarisha ulinzi na usalama katika mipaka ya vyuo kwa kuweka uzio.
v. Kuweka kanuni zinazozuia upitaji holela katika maeneo ya chuo.
vi. Kuweka kipaumbele cha upatikanaji wa huduma za malazi ndani ya vyuo ili kuwalinda wasichana, wanawake na watu wenye ulemavu.
vii. Kuwashirikisha wazazi/walezi na wadau wengine katika kuanzisha/ kuimarisha mikakati ya ulinzi na usalama dhidi ya ukatili na unyanyasaji.
viii. Kuanzisha/kuimarisha dawati la jinsia litakaloshughulikia maswala ya ulinzi na Usalama
ix. Kuandaa na kuipa kipaumbele ajenda ya ulinzi na usalama katika mikutano mbalimbali inayofanyika vyuoni ikiwemo Mabaraza ili kujadili namna ya kuzuia ukatili wa kijinsia na aina zote za unyanyasaji.
x. Kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa ulinzi na usalama vyuoni ikiwa ni pamoja na kuanzisha na kuwezesha mafunzo kwa timu jumuishi ya ulinzi na usalama.

**3.2 Lengo la 2: Kuanzisha/kuboresha huduma saidizi zitakazowezesha kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama.**

**Maelezo ya Lengo**

Vyuo viwe na huduma saidizi na utaratibu wa haraka wa kukabiliana na viashiria, vitendo na washukiwa wa ukatili ili kuhakikisha usalama wa wanachuo. Hivyo, huduma saidizi zinapaswa kuboreshwa ili kutoa msaada wa haraka wakati wa matukio au wasiwasi kuhusu ulinzi na usalama.

**Mkakati 1: Kuanzisha/ kuboresha Huduma ya Ushauri na Unasihi**

**Tamko la mkakati**

Utoaji wa huduma ya ushauri na unasihi vyuoni husaidia katika kukuza ulinzi, usalama na maendeleo ya kihisia miongoni mwa waathirika wa ukatili vyuoni. Hivyo, vyuo vinapaswa kuzingatia yafuatayo: -

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. Kuanzisha/ kuimarisha vitengo vya ushauri na unasihi kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa wanachuo.
ii. Kuanzisha/ kuimarisha programu za elimu rika juu ya Stadi za Maisha, Afya ya uzazi, Magonjwa yasiyo ya kuambukiza na magonjwa ya kuambukiza kama vile Virusi Vya Ukimwi (VVU) vilabu vya wanachuo na michezo kwa kujumuisha shughuli zote hizi katika ratiba ya vyuo.
iii. Kuhamasisha wanachuo, wazazi / walezi na jamii juu ya masuala yanayohusiana na ukatili dhidi ya watoto, wanawake, vijana, na wenye ulemavu.
iv. Kushirikisha wazazi / walezi na jamii juu ya ajenda ya ulinzi na usalama wa wanachuo kupitia matukio ya mara kwa mara kama vile mahafali.
v. Kushirikisha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika ngazi za chini ili kutambua matukio, kubuni mbinu za kutatua changamoto za masuala ya ulinzi na usalama.
vi. Kujenga uhusiano mzuri na uaminifu kati ya wanachuo na jamii inayozunguka vyuo.
vii. Kuimarisha mfumo wa rufaa kwa wahanga wa vitendo vya ukatili.

**Mkakati 2: Kuimarisha dawati la jinsia vyuoni**

**Tamko la mkakati**

Ili kushughulikia masuala ya ukatili wa kijinsia, dawati la jinsia linapaswa kuanzishwa na kuimarishwa ipasavyo pamoja na kubuni mbinu za kuelimisha wanachuo, watumishi, na wadau wengine kuhusu ulinzi na usalama vyuoni.

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. Kuhamasisha utekelezaji wa miongozo ya dawati la jinsia vyuoni
ii. Kupokea na kuchakata ripoti zote za Ukatili wa Kijinsia katika Vyuo.
iii. Kutoa msaada wa kisaikolojia kwa wahanga wa Unyanyasaji wa Kijinsia.
iv. Kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali

v. Kufuatilia na kupokea taarifa kuhusu matukio na rufaa mbalimbali zinazohusiana na ukatili wa kijinsia vyuoni.

vi. Kuzingatia utekelezaji wa masuala ya kijinsia katika Sera, Mipango, Miradi, Mikakati, Miongozo na Bajeti za Vyuo.

vii. Kuelimisha Jamii ya chuo husika kuhusu Ukatili wa Kijinsia pamoja na kuzingatia masuala mbalimbali ya kijinsia katika utekelezaji wa majukumu na wajibu.

viii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa masuala ya ukatili wa kijinsia na kuchochea mwenendo wa tafiti mbalimbali kuhusu masuala ya Ukatili wa Kijinsia ndani na nje ya Chuo.

ix. Kuandaa na kutunza kumbukumbu za masuala ya kijinsia yaliyoripotiwa kwenye Dawati.

x. Kuandaa na kuwasilisha taarifa za robo mwakakuhusu utekelezaji wa majukumu ya Dawati pamoja na utekelezaji wa Mpango Kazi katika mamlaka za vyuo.

xi. Kuimarisha mafunzo ya ndani kuhusu masuala mtambuka yanayojitokeza katika dawati la jinsia .

xii. Kuunganisha wahanga wa ukatili wa kijinsia na mamlaka zingine zinazohusika na masuala hayo hususani Ofisi ya Ustawi wa Jamii au vyombo vya uchunguzi kama vile Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali; na

xiii. Kufuatilia kwa karibu uchunguzi wa masuala ya ukatili na kutunza kumbukumbu za siri za ushahidi wa matukio husika.

**3.3 Lengo la 3: Kuanzisha mfumo wa kukabiliana na ukatili kupitia taratibu salama za kutoa taarifa.**

**Maelezo ya Lengo**

Mfumo wa kukabiliana na ukatili pamoja na utoaji wa taarifa za ulinzi na usalama una njia kadhaa zinazotegemeana**.** Hivyo,vyuo vinaelekezwa kujumuisha masuala ya ulinzi na usalama kwenye mpango mkakati na mpango kazi. Mifumo hiyo itahakikisha utoaji wa taarifa za ulinzi na usalama inafanyika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za uendeshaji wa vyuo.

**Mkakati 1: Kuanzisha mfumo wa kukabiliana na ukatili.**

**Tamko la Mkakati**

Mfumo wa wazi wa kukabiliana na ukatili vyuoni ni nyenzo muhimu inayowawezesha wahanga wa ukatili kupata msaada stahiki kwa wakati ili kutatua changamoto zinazowakabili.

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. **Kutambua:** Watumishi, wanachuo na jamii wajengewe uelewa kuhusu aina zote za ukatili na unyanyasaji na namna ya kutoa taarifa kwa kuzingatia Miongozo ya Dawati la Jinsia.

ii. **Kutunza kumbukumbu**: Taarifa zote za matukio zinazohusu unyanyasaji na ukatili zinapaswa kuandikwa na kutunzwa kwa kuzingatia usiri.

iii. **Kushughulikia tuhuma za unyanyasaji:** Katika kushughulikia tuhuma za unyanyasaji, taratibu za kinidhamu zifuatwe ipasavyo. Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya mtuhumiwa baada ya ushahidi kuthibitishwa kwa uhakika kuwa anahusika na unyanyasaji huo.

iv. **Kuzuia na kukabiliana na uonevu:** Uongozi wa vyuo unapaswa kujenga uelewa kwa wanachuo, watumishi, bodi za vyuo na wadau wengine ili kuwawezesha kutoa taarifa za matukio mbalimbali ya uonevu pamoja na njia bora za kukabiliana na hali hiyo.

v. **Kutambua na kushughulikia unyanyasaji wa mtandaoni.** Uongozi wa vyuo unapaswa kuwapa wadau wote taarifa muhimu kuhusu unyanyasaji wa mtandaoni na njia sahihi ya kutoa taarifa. Hii inaweza kufanyika kupitia mikutano, vipindi vya darasani, vilabu, magazeti ya vyuo au matangazo.

vi. **Kuongeza uelewa wa Sheria ya Makosa ya Mtandao (2015**). Kuelimisha jamii ya chuo kuhusu Sheria ya Makosa ya mtandao (2015) na kuchukua hatua stahiki ili kutokomeza uonevu wa mtandaoni. Ongezeko la uelewa litawezasha matumizi sahihi ya mitandao kwa kuhakikisha kuwa picha, na taarifa binafsi za wanachuo zinahifadhiwa na kutumika ipasavyo.

**Mkakati wa 2: Kuanzisha/kuboresha mfumo salama wa kutoa taarifa.**

**Tamko la Mkakati**

Utaratibu salama wa kutoa taarifa sahihi ni muhimu kwa vyuo ili kuzuia na kukabiliana na matukio ya unyanyasaji na ukatili. Hivyo, mikakati tofauti inahitajika kwa wanachuo ili kutoa taarifa kwa usalama kuhusu vitisho, vurugu, ukatili, au wasiwasi kuhusu usalama wao.

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. **Kutoa taarifa kupitia mfumo wa uongozi uliowekwa:** Baada ya tuhuma na malalamiko kuripotiwa kwa wasimamizi wao, mhusika anatakiwa kufanyia kazi taarifa mara moja na kwa haki.

ii. **Kutoa taarifa bila kupitia mfumo wa uongozi uliowekwa:** Mwanachuo awe huru kutoa taarifa kwa mwanachuo mwenzake, mtumishi, au chombo/kamati anachokiamini,kuhusu malalamiko au wasiwasi juu usalama wake. Kwa mfano, anaweza kuwasiliana na chombo/kamati inayohusika (Kamati za Maadili) moja kwa moja. Chombo/kamati lazima iwe na namba ya simu na barua pepe zinazopatikana.

iii. **Kutoa taarifa kwa siri:** Kuhakikisha kwamba watumishi na wanachuo wanahimizwa kuibua taarifa za matukio au wasiwasi wowote juu ya usalama wao kwa wakati na usiri. Hata hivyo hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mtu yeyote anayetoa taarifa zisizo sahihi na za kupotosha kwa nia ya kuharibu taswira ya mtu mwingine.

iv. **Kuibua wasiwasi/ tuhuma:** Kuwasilisha taarifa ya ulinzi na usalama kupitia utaratibu uliowekwa ikiwa ni pamoja na sanduku maalumu la maoni ambalo litakuwa chini ya usimamizi wa dawati la jinsia. Sanduku hili linanapaswa kufuguliwa kila siku.

**Mkakati wa 3: Kuboresha ushirikiano, utoaji wa taarifa na taratibu za rufaa ili kulinda wanachuo hasa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu kwa lengo la kuimarisha ustawi, afya, ulinzi na usalama wao.**

**Tamko la Mkakati**

Wadau wanatekeleza majukumu mbalimbali katika kukuza usalama na ustawi wa wanachuo. Taratibu madhubuti zinapaswa kuwekwa ili kuimarisha ushirikiano endelevu kati ya wadau. Hivyo, kwa kushirikiana na wadau wengine vyuo vitakuwa na fursa ya kuratibu juhudi za kukuza ulinzi, usalama na ustawi chuoni.

**Maelekezo ya kutekeleza Mkakati**

i. Uongozi wa vyuo unapaswa kutambua na kudumisha ushirikiano na mashirika, idara na watoa huduma ambao wanaweza kutoa msaada juu ya masuala ya ulinzi na usalama. Taasisi hizo ni pamoja na hospitali, kituo cha polisi, kitengo cha msaada wa kisaikolojia, Asasi za Kijamii (AZAKI) na mashirika mengine yasiyo ya Serikali, huduma za msaada za mtandaoni, msaada wa mawasiliano mtandaoni, kamati tofauti, na dawati la jinsia.

ii. Uongozi wa vyuo utahakikisha upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza na miongozo yake ya uendeshaji pamoja na kutoa mafunzo kwa jumuiya juu ya matumizi sahihi ya vifaa vya huduma ya kwanza.

iii. Mamlaka husika kuhakikisha uwepo wa mtaalamu wa huduma ya afya na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa na dawa muhimu za kutosha ili kutoa matibabu kwa wakati kwa wahanga.

**3.4 Lengo 4: Kujenga uelewa juu ya masuala ya ulinzi na usalama kwa wadau wote wenye mahusiano ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja na wanachuo.**

**Mkakati: Kuongeza uelewa ili kuhakikisha kuwa wadau wanawezeshwa na kuhimizwa kutambua na kuzuia unyanyasaji na ukatili.**

**Tamko la Mkakati**

Uelewa na uwezeshaji mdogo kuhusu ulinzi na usalama umesababisha kukua kwa unyanyasaji na ukatili katika vyuo na jamii kwa ujumla. Hivyo, mikakati ya kujenga uelewa na uwezeshaji itatoa fursa kwa wanachuo, watumishi, uongozi, bodi, wazazi, jamii na wadau wengine kujifunza na kuzuia aina zote za ukatili na unyanyasaji vyuoni.

# SURA YA NNE

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Sura hii inahusu mifumo na taratibu za usimamizi wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama. Aidha, inafafanua michakato na taratibu za utoaji wa taarifa kwa kushirikiana na mamlaka husika, wadau, pamoja na majukumu yao.

### 4.1 Mifumo ya Usimamizi na taratibu za Ulinzi, usalama.

Mifumo ya simamizi na taratibu za Ulinzi na usalama zinafafanua mambo yanayohitajika kutolewa taarifa kwenye masuala ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na mamlaka husika. Hii itafanyika kupitia:

i. **Mashirika mbalimbali:** Kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali kama vile Afya, Polisi, Ustawi wa jamii, Maendeleo ya jamii, Dawati la jinsia na Vilabu vya wanachuo ili kukuza ustawi wa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu na kuwalinda dhidi ya Ukatili wa kijinsia.

ii. **Ufuatiliaji na tathmini:** Kujumuisha utekelezaji wa mwongozo wa ulinzi na usalama katika mpango wa usimamizi kwa mujibu wa mpango mkakati wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

iii. **Mafunzo kwa watumishi na uongozi**: Kuhakikisha kuwa watumishi wote na jamii wanapata mafunzo husika ili kuongeza maarifa na ujuzi pamoja na kubadili mitazamo ya kutoa huduma sahihi na ulinzi kwa wanachuo na jamii kwa ujumla.

iv. **Utekelezaji wa taratibu za ulinzi na usalama kwa wazazi, watumishi na wadau wengine**: Kuongeza uelewa juu ya mwongozo, kwa kuwafundisha kutambua tabia zisizofaa na kuhakikisha upatikanaji wa mwongozo kupitia tovuti na maktaba za taasisi.

v. **Kuhuisha mwongozo wa ulinzi na usalama:** Mwongozo utahuishwa kuendana na mabadiliko yanayojitokeza pamoja na kuwajengea uwezo watumiaji na wadau.

### 4.2 Majukumu na Wajibu wa Wadau.

Yafuatayo ni majukumu ya wadau mbalimbali katika kutekeleza Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi, Vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu.

#### 4.2.1 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

i. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
ii. Kuhimiza matumizi ya sheria, taratibu, kanuni na miongozo ya elimu itakayowezesha utekelezaji thabiti wa Mwongozo wa ulinzi na usalama katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi,Vyuo Mafunzo ya Ufundi Stadi na Vyuo vya Ualimu.
iii. Kuratibu upatikanaji wa zana na vifaa vya mafunzo juu ya mwongozo wa ulinzi na usalama.
iv. Kuwajengea uwezo watekelezaji kuhusu Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
v. Kutenga rasilimali na kuhamasisha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
vi. Kufuatilia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za Mwongozo wa Ulinzi na Usalama ili kufanya maamuzi stahiki ya kisera.
vii. Kusambaza Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa wadau.
viii. Kujumuisha masuala ya ulinzi na usalama kwenye Mpango Mkakati wa Wizara.
ix. Kujumuisha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwenye mipango ya ukaguzi wa ndani.

#### 4.2.2 Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI)

i. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.
ii. Kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

#### 4.2.3 Bodi za Vyuo

i. Kusimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika vyuo na jamii inayozunguka.
ii. Kutoa ushauri juu ya masuala yanayohusiana na utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
iii. Kutambua na kupendekeza maeneo ya ushirikiano na mashirika mengine katika utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na usalama.

#### 4.2.4 Mamlaka za Serikali za Mitaa

i. Kutekeleza malengo na mikakati yote ya Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika maeneo yao ya kazi.
ii. Kujumuisha utekelezaji wa shughuli za ulinzi na usalama katika mipango na bajeti za Serikali za Mitaa.
iii. Kuhamasisha mashirika yasiyo ya kiserikali, Asasi za Kijamii na Mashirika ya Kidini kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kuendana na mipango ya Mamlaka za Serikali za Mitaa.
iv. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
v. Kujenga uelewa kwa jamii juu ya umuhimu wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu na kuwaunganisha na msaada unaohitajika.
vi. Kutoa ushauri na msaada wa kisaikolojia kwa wahanga wa Ukatili wa kijinsia katika jamii.

#### 4.2.5 Menejimenti za vyuo

i. Kutekeleza Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
ii. Kushirikisha wazazi / walezi na jamii ili kuwezesha utekelezaji wa malengo ya Mwongozo wa Ulinzi na usalama.
iii. Kuhuisha na kuimarisha uongozi jumuishi wa wanachuo.
iv. Kuratibu utendaji wa idara za utawala wa vyuo ikiwa ni pamoja na uongozi wa Wanachuo katika kutekeleza Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.

v. Kushirikiana na wadau wengine kama Serikali za Mitaa na Asasi zisizo za Kiserikali ili kupanga na kusimamia utekelezaji wa mipango ya elimu rika ndani na nje ya vyuo.
vi. Kusimamia maadili ya utumishi wa umma, miongozo, kanuni na taratibu kwa watumishi.
vii. Kutoa taarifa za utovu wa nidhamu na ukiukwaji wa Mwongozo wa Ulinzi na usalama kwa mamlaka husika.
viii. Kutenga rasilimali za utekelezaji wa Mwongozo

### 4.2.6 Washirika wa Maendeleo

i. Kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama kwa kutenga rasilimali.
ii. Kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuwezesha mifumo madhubuti juu ya utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.

### 4.2.7 Mashirika yasiyo ya Kiserikali

i. Kufanya kazi kwa kushirikiana na Serikali/vyuo ili kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
ii. Kuhamasisha na kutenga rasilimali ili kuwezesha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama vyuoni.

### 4.2.8 Sekta Binafsi

i. Kutoa msaada wa rasilimali katika utekelezaji wa Mwongozo wa ulinzi na usalama.
ii. Kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa kuwalinda wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

### 4.2.9 Wazazi/Walezi na Jamii

i. Kutoa elimu juu ya Mwongozo wa Ulinzi na Usalama katika ngazi ya familia na jamii.
ii. Kushirikiana na vyuo katika uendeshaji wa shughuli za Ulinzi na Usalama.
iii. Kuweka mazingira rafiki yatakayowezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu wanakuwa salama na wanapata elimu bora.

#### 4.2.10 Watumishi wa Vyuo

i. Kutekeleza Mwongozo wa Ulinzi na Usalama
ii. Kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na maadili ya utumishi wa umma wakati wa kutekeleza majukumu.
iii. Kushirikiana na uongozi wa chuo katika kukabiliana na masuala yanayohatarisha ulinzi na usalama katika Chuo.

#### 4.2.11 Uongozi wa Wanachuo

i. Kuunda uongozi shirikishi unaozingatia makundi mbalimbali ya wanachuo.
ii. Kuzingatia maoni ya wanachuo katika kufanya maamuzi.
iii. Kutoa mrejesho kwa wanachuo juu ya majadiliano na maamuzi yaliyofikiwa kwenye mikutano kuhusu masuala ya ulinzi na usalama.
iv. Kutoa mafunzo elekezi kwa viongozi wapya wa wanachuo waliochaguliwa juu ya mambo muhimu ya mwongozo wa ulinzi na usalama, majukumu na wajibu wao katika kuboresha mazingira salama ya kujifunzia vyuoni.
v. Kupendekeza kwa uongozi wa chuo hatua za kuondokana na changamoto za ulinzi na usalama zinazowakabili wanachuo juu ya aina nyingine za ukatili na unyanyasaji.

#### 4.2.12 Mwanachuo

i. Kuzingatia maelekezo ya Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.
ii. Kuhamasisha na kushiriki katika programu mbalimbali za ulinzi na usalama vyuoni.
iii. Kuepuka tabia na maeneo hatarishi ndani na nje ya vyuo.
iv. Kutambua na kulinda thamani ya utu wao.
v. Kutoa mapendekezo kwa uongozi wa chuo na serikali ya wanachuo kuhusu namna bora ya kushughulikia vitendo vya ukatili na unyanyasaji.
vi. Kuchagua wajumbe miongoni mwao ili kushiriki katika timu jumuishi vyuoni.
vii. Kutoa taarifa sahihi na kwa wakati kwa mamlaka husika kuhusu viashiria au matukio ya ukatili na unyanyasaji.

# SURA YA TANO

## 5.0 Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji

Ufuatiliaji, Tathmini na Ujifunzaji ni mfumo au utaratibu muhimu utaotumika kusimamia na kupima maendeleo ya utekelezaji wa mwongozo katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mfumo huu pia utatumika kupima uwajibikaji na ujifunzaji kwa wadau wanaohusika katika ulinzi na usalama wa wanawake, wasichana, vijana, na watu wenye ulemavu katika Vyuo. Hivyo, Ufuatiliaji,Tathmini na Ujifunzaji katika utekelezaji wa mwongozo huu ni muhimu ili kufahamu kiwango cha matokeo ya malengo yaliyokusudiwa.

## 5.1 Ufuatiliaji na Utoaji wa Taarifa

Ufuatiliaji wa utekelezaji wa mwongozo huu utakuwa endelevu na taarifa zitatolewa na mamlaka husika. Ufuatiliaji utafanywa kila robo ya mwaka na halmashauri na Vyuo. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itafanya ufuatiliaji mara mbili kwa mwaka. Ripoti za maendeleo ya utekelezaji wa mwongozo zitaandaliwa kila robo ya mwaka na zitajumuishwa katika ripoti ya mwaka ya wizara.

Mchakato wa ufuatiliaji utahusisha zana mbalimbali za kukusanya, kuchambua na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama. Vyuo na Halmashauri zitatoa taarifa za kila robo mwaka zitakazoonyesha maendeleo ya utekelezaji wa mwongozo katika maeneo yao.Taarifa ya mwisho ya mwaka itaandaliwa na kusambazwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau.

## 5.2 Tathmini

Tathmini itafanyika ili kupima **ufanisi, athari na uendelevu** wa utekelezaji wa malengo na matokeo ya Mwongozo wa Ulinzi na Usalama. Tathmini itafanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau kila baada ya miaka mitatu ili kupima ufanisi wa utekelezaji mwongozo. Hii itatoa fursa ya kuhuisha mwongozo kulingana na mahitaji ya wakati husika.

Tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa mwongozo itatoa mapendekezo ya kimkakati na kiutendaji pamoja na kuonesha uzoefu uliopatikana katika kuwezesha mipango ya kila Chuo kulingana na malengo yaliyokusudiwa.

### 5.3 Ujifunzaji

Vikao vya tafakuri vitafanywa mara moja kwa mwaka na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Washirika wa Maendeleo na Vyuo ili kubadilishana uzoefu na kupitia taarifa za ufuatiliaji na tathmini ili kufanya maamuzi sahihi juu ya mafanikio na nini kinahitaji mabadiliko katika kuboresha utekelezaji wa Mwongozo wa Ulinzi na Usalama.

**KIAMBATISHO 1: MPANGO WA UFUATILIAJI, TATHMINI NA UJIFUNZAJI.**

**MATOKEO: Kupungua kwa Vitendo vya Ukatili na Unyanyasaji Vyuoni**

| Lengo | Matokeo ya kimkakati | Viashiria | Shughuli | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| 1. Kuimarisha ulinzi na usalama wa wanachuo dhidi ya unyanyasaji na ukatili. | 1.1. Kuimarika kwa ulinzi na usalama wa wanachuo dhidi ya unyanyasaji na ukatili. | 1.1.1 Idadi ya nakala za mwongozo wa ulinzi na usalama zilizosambazwa. | 1.1.1.1 Kusambaza nakala za mwongozo wa ulinzi na usalama katika Vyuo. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |
| | | 1.1.2 Idadi ya Vyuo vilivyoanzisha na kufunza timu za ulinzi na usalama | 1.1.2.1 Kuanzisha timu jumuishi za ulinzi na usalama. | Chuo |
| | | | 1.1.2.2 Kutoa mafunzo kwa timu jumuishi za ulinzi na usalama. | |
| | | 1.1.3 Idadi ya vikao viliyofanyika kujadili masuala ya ulinzi, usalama na ukatili wa kijinsia. | 1.1.3.1 Kuandaa na kuwasilisha ajenda ya ulinzi na usalama katika vikao vya wanachuo | Chuo |

| Lengo | Matokeo ya kimkakati | Viashiria | Shughuli | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| | | | (kujadili masuala ya kuzuia Ukatili wa Kijinsia. | |
| 2. Kuanzisha / kuboresha huduma saidizi za kushughulikia masuala ya ulinzi na usalama. | 2.1 Kuimarika kwa uwezo wa mifumo ya utoaji taarifa na huduma saidizi ili kukabiliana na ukatili. | 2.1.1 Idadi ya vyuo vilivyoanzisha/kuimarisha vitengo vya huduma saidizi. | 2.1.1.1 Kuanzisha / kuimarisha vitengo vya mwongozo na ushauri vyuoni | Chuo |
| | | 2.1.2 Idadi ya watumishi na wanachuo waliopata huduma ya ushauri na unasihi. | 2.1.2.1 Kutoa ushauri na unasahi kwa watumishi na wanachuo wanaohitaji msaada. | Chuo |
| | | 2.1.3 Idadi ya Vyuo vilivyoanzisha Dawati la Jinsia na linafanya kazi. | 2.1.3.1 Kuanzisha na kuendesha Dawati la Jinsia Vyuoni | Chuo |

| Lengo | Matokeo ya kimkakati | Viashiria | Shughuli | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| | | 2.1.4 Idadi ya Vyuo vilivyo na Dawati la Jinsia lenye wahusika waliopatiwa mafunzo. | 2.1.4.1 Kutoa mafunzo kwa wahusika wa Dawati la Jinsia | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. |
| 3.Kuanzisha/kuimarisha mfumo wa kukabiliana na unyanyasaji na ukatili kupitia mfumo salama wa kutoa taarifa. | 3.1 Kuimarika kwa Mfumo wa utoaji taarifa za kukabiliana na unyanyasaji na ukatili. | 3.1.1 Idadi ya wanajamii, wanachuo na watumishi wa Vyuo waliopata mafunzo ya kutambua na kuripoti matukio ya unyanyasaji na ukatili. | 3.1.1.1 Kutoa mafunzo kwa wanachuo, watumishi na jamii ya namna ya kutambua na kutoa taarifa za matukio ya unyanyasaji na ukatili. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, |
| | | 3.1.2 Idadi ya mitandao iliyoanzishwa kwa ajili ya ushirikiano na rufaa. | 3.1.2.1 Kuanzisha mahusiano na mashirika na wadau . | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Vyuo, Mashirika yasiyo ya Kiserikali. |
| | | 3.1.3 Idadi ya matukio ya ukatili yaliyoripotiwa na kuhifadhiwa kwenye kumbukumbu. | 3.1.3.1 Kuhifadhi kumbukumbu za matukio ya ukatili na unyanyasaji | Chuo |

| Lengo | Matokeo ya kimkakati | Viashiria | Shughuli | Mhusika |
|---|---|---|---|---|
| 4. Kujenga uelewa wa masuala ya ulinzi na usalama kwa wadau wenye mawasiliano ya moja kwa moja au yasiyo ya moja kwa moja na vyuo. | 4.1 Kuongezeka kwa uelewa kwa wanajamii kuhusu masuala ya ulinzi na usalama. | 4.1.1 Idadi ya kampeni, makongamano, na midahalo na michezo iliyofanyika ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii. | 4.1.1.1 Kuandaa na kufanya kampeni, makongamano, midahalo na michezo ili kuwasilisha ujumbe kwa jamii. | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, OR-TAMISEMI, na Wadau. |
| | | 4.1.2 Idadi ya mikutano inayofanyika na wanajamii juu ya masuala ya ulinzi, usalama, na maendeleo ya wanachuo | 4.1.2.1 Kufanya mikutano na wanajamii kuhusu masuala ya ulinzi, usalama, na maendeleo ya wanachuo | Chuo |

KATIBU MKUU

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, NA TEKNOLOJIA

Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya,
S.L.P 10, 40479 Dodoma, Tanzania.
Barua pepe: info@moe.go.tz
Tovuti: http://www.moe.go.tz

In partnership with Canada

COLLEGES & INSTITUTES CANADA

Tanzania Empowerment through Skills Program

TESP